Ukiangalia hospitali, haikuwa imetengewa pesa ya madawa lakini hili Bunge limejaribu sana kutoa pesa na kuweka kwa mahospitali ili watu wapate madawa. Kwa hivyo Waheshimiwa wamepitia hii bajeti vizuri. Ukiangalia mambo ya elimu, hawakuwa wametengea watoto wa maskini pesa ya ufadhili na unajua katika hii Laikipia sisi zote sio sawa. Kama mahali nimetoka huko Sosian, watu wengi ni maskini na wanaendelea kusomea chini ya miti. Hata pesa ya kujenga darasa ya mtoto wa chekechea haikuwa imewekwa.

Kwa hivyo, hili Bunge limefanya kazi ya maana kwa kupitia kwa njia nzuri na kuhakikisha ya kwamba hawa watu wamepata pesa ya *bursary* na madawa na madarasa ya ECDE. Kuna pesa ya NHIF ambayo tunatenga na kusema ya kwamba kila wakati watu

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

walipiwe. Hata ukienda katika wadi yangu hakuna mtu hata siku moja niliwahi kusikia amelipiwa hizo pesa. Hawa watu wameangalia ukweli kabisa na tumeitisha hii ripoti hapa kwa muda na haikuwa inaletwa kwa sababu walikuwa wanajua ya kwamba hakuna kazi ambayo wamefanya.

Bi. Spika, mimi naunga hii ripoti mkono na sitaongea mengi lakini tutahakikisha ya kwamba hili Bunge litaendelea kusimama vile limesimama siku ya leo na tutafanya kazi kwa wanjiku kwa sababu hao ndio wametutuma hapa kwa ile njia inayofaa na waridhike. Asante.

Hon. Catherine Kibue: Asante sana, Bi. Spika kwa kunipa fursa hii. Kwanza nataka nipongeze Kamati ya Bajeti na niwape heko. Nataka niseme ya kwamba hata kama Mzungu husema hata kama ishapita, hata afadhali tungekuwa tumejua hapo awali. Hiyo kamati ndiyo tungepatia bajeti na hatungekuwa tumepitwa na muda.

Niwashukuru nyinyi wote Kamati ya Bajeti kwa kuona umuhimu wa kuangalia watoto na kurudisha *bursary* na pia kuona umuhimu wa kujenga darasa za chekechea ndio watoto wapate mahali pa kusomea. Kama vile Mheshimiwa Jacob amesema, waache kusomea chini ya miti. Pia nataka nishukuru kamati tena kwa kuona umuhimu wa kuondolea wanalaikipia mzigo wa deni ambao ungewalemea kwa miaka mingi. Kama Wabunge wa Laikipia, tungepeta laana kutoka kwa wakaaji wa Laikipia kwa sababu kuna shida nyingi sana kama za Korona na hata zile vidonda ambazo ziko katika roho zao hawajapona na kisha tuwaongezee mizigo ya kulipa deni.

Kwa hivyo nataka niwashukuru sana na niwaambie tuendelee hivyo. Ningetaka Mwenyekiti wa Bajeti ukimalizia, mimi ni mkaaji wa Ngobit na hata kama Mheshimiwa wa eneo hilo hayuko, ningetaka kujua kwa sababu sijaona barabara za Ngobit ama tulisahaulika ama tulitoka Laikipia, uweze kutujibu. Asante.

Hon. Daniel Mugweru: Thank you, Mr. Speaker for giving me this chance to make my contribution towards this report on budget. Madam Speaker, we as Hon. Members in this House represent thousands of people who are out there. The obligations that we have is to protect their interests, to fight for their rights and to fulfil the promises we made to the people of Laikipia. When we have a budget that has the interest of Laikipians, it is one of the best things that we can do because the people of Laikipia are expecting us to perform.

Madam Speaker, I wish to thank the Budget Committee for coming up with such a report and all the departments have been considered greatly because the report that has been made by the Budget Committee has come from the Sectorial Committees and they are comprised of all the Members of this House. This means that every corner of Laikipia is included in this budget.

Madam Speaker, anything that is not in this budget is either the Member who represents that area was not keen in doing that because we are compiling a report coming from the sectorial committees which are comprised of all these Members who are here. Madam Speaker, the budget that we have cuts across the Laikipia and all departments. If you look at the Department of Health which has been on the limelight in this country because of poor health, the committee was able to allocate funds to purchase drugs for the NTRH hospital. Each had zero allocation.

So we failed to understand why we should have zero shillings allocation for drugs for such a big hospital. I wish to thank the Budget Committee for seeing the importance of having drugs in that hospital noting that the same hospital is the one that supplies the drugs to the

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

dispensaries around these health centres. When we do not have a budget for drugs for NTRH, it means that the dispensaries around and the health centres that we have will not have drugs.

Therefore, having the Budget Committee finding it wise to invest in health and create funds for drugs is one of the best things that could have happen to the people of Laikipia. I am sure the people of Laikipia will celebrate hearing that they have drugs in their hospitals. Madam Speaker, the decision of the reduction of NHIF was informed because the Members who represent the people of Laikipia are categorical.

The registered people to benefit from this fund are not well known to the Members. We do not know the people who are supposed to benefit and the list we have, the people who were registered two years ago have never benefited until today. Madam Speaker, we cannot sit down and set the budget whereas the people who are registered do not benefit from the same. Every day you will find people coming to our houses claiming that we were registered and we are going to get free NHIF only to go to hospital and find arrears since the day they were registered.

No single shilling has ever been paid. Madam Speaker, sometimes we should not set funds so that we may be found that we have set funds. We set funds to be utilised by the people of Laikipia. We found it unnecessary to have that fund if it is not helping the people of Laikipia. To replace it, we found it wise to stop that fund and put it in purchasing of our drugs in our hospitals. Madam Speaker it is not only the NTRH, if you go through the budget, all the wards that are represented in this House, the dispensaries that are in those areas are either benefitting maybe in improving theatres or infrastructures.

If you go to Umande we are doing a new dispensary at Maili nane. All the members who represent the people of Laikipia, the interest of the people they represent are catered for. If you go to the Infrastructure Department which has benefitted largely, it is very clear that the biggest challenge in Laikipia is infrastructure. We need to do all weather roads in Laikipia so that we may enable our people travel from one place to the other.

Madam Speaker, when we have good weather roads in Laikipia I believe it will open up business in this county and we are going to generate more revenue which will help us do more in future. Madam Speaker, we want to improve the lives of the people of Laikipia by improving their roads. The Members who have contributed have mentioned about bursaries. The whole world has been going through COVID and many of us especially parents are waking up working hard and we as the people of Laikipia apart from the COVID-19, we have been affected by drought.

We can tell by the look of things that next year there will be famine in this county. The little money that our people will get will go to feed their families and probably most of our students will drop out from schools. When we find that we have a budget that has only 25 million for bursary, we felt that it was wise to double that money or give more so that our students may benefit from this kitty so that we help them at this hour of need.

Madam Speaker, the Hon. Members from Laikipia North continue to say that there are children learning under the trees. I do not want to go that route because they need to do something beyond that. We need to hear that young pupil's classes are in a Manyatta or a mud class so that when we go there we improve what the community has done. Having said that, that doesn't mean that we are not supposed to construct classes in their areas. That is why we have set a budget to do classes in every ward.

So every ward will benefit from this just as they will benefit from bursaries. Madam Speaker, if you go to the Water Department and everybody knows that there has been drought

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

in this county. Madam Speaker, our rivers have dried up and now it is our responsibility to make sure that our people access clean water in every corner of this county. That is why the Department of Water has benefitted from a huge budget so that we improve the boreholes that we have. It is unfortunate that until today, we have boreholes that are operated manually yet we are saying there is a lot of drought.

Our areas have been blessed with a lot of Sun and we need to equip all boreholes in this county with solar panels so that as much as we would say there is drought, our people will be able to access clean water which is their rights. Madam Speaker, the Budget Committee found it necessary to put a lot of money in the Water Department to either equip boreholes, drill new boreholes and the water projects that are in our area to benefit from pipes, storage tanks and all that.

Madam Speaker, it is the high time we give priority and we put a lot of money to the priorities of this county. If you go to the Department of Trade, businesses in Laikipia have been hit hard by COVID. We have set money to help improve business in this county. If you go to markets in this area and an example is like Mugumo market where we have thousands of people going to that market if there is rain; I do not know where those people will go. The markets that we are calling markets are on a swampy area.

If it rains there will be no market in Mugumo. We have set funds in that department to gravel that market and improve it into standards so that we give our business people good atmosphere to do their business. This is one of the best budgets that the people of Laikipia will enjoy. As the Hon. Chair has just said, we have done our part. I am sure members will support this report. I am sure we are going to adopt it and the next step will be our responsibility to do our part and give the next person do his part because the Constitution has given us different mandates.

Madam Speaker, we have done our part, we expect the budget to decide and the people of Laikipia will benefit from this budget because it is not just reading the budget and going through what has been written but the issue is implementation. This budget if well implemented being our last year, I am sure the people of Laikipia will be able to benefit from it and will be able to truly say we had a government of 2017-2022. Thank you, Madam Speaker. I support.

Hon. George Karuiru: Thank you, Madam Speaker. I rise to support the report on the Laikipia County Budget Estimates for the Financial Year 2021/2022. First of all, I would like to congratulate the newly elected Chairperson of the Budget Committee, Hon. Stephen Ndiritu. I would want to urge him and the committee that budget matters are not matters to joke with. With the little time that he has been the chair, we can see the impact he has made in the Budget Committee.

Madam Speaker, I will touch on the leasing programme and the Hon. Members are witnesses that there has been poor management in the leasing programme. Madam Speaker, I will not say that slashing some money in the leasing programme is due to poor programme but I heard Hon. Meshami quoting that this year he got a leased machine. It is very worrying because of the poor management of the leasing programme. For example, the leased machines are doing work in Igwamiti for one year while other areas have not been touched.

I think there should be an improvement. I know we have people who are equal to the task. We are told of lack of fuel yet those tracks are put somewhere and are not working. They should be checked and I urge the Committee on Infrastructure to give us a programme as Hon. Members so that we know where the machines are going and what they are doing so that we see the benefits of the leasing programme.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Madam Speaker, the other one is about the fast tracking of the programmes that we have in this budget. We are in July and we are expecting that next week, H.E the Governor will sign this budget. Because we have all the machinery to contract programmes in this budget, this should be implemented immediately. I am not saying that we need sun but God is for us all who is the facilitator of Sun and Rain.

Madam Speaker, I know if it is tracked, infrastructural projects should be fast tracked. The other one is about the transparency in budget transmission. Yesterday the former Chair of the Budget Committee said that he has two budgets. This is an Honourable House, so I wonder how the second budget was slotted in here. There is a process from the Executive to the Assembly. Now that we have an able Chair who cannot be compromised we expect that the budgets will be transparent and they will be implemented.

On the issue of bursaries, we gave a three-quarter of the 2019/2020 bursary. The other quarter might be delivered and it is very worrying that we did not feel the Wanjiku yet we are always being disturbed as MCAs. I and other Hon. Members know that when we are at home we must have 10 to 20 litres of milk now that children are about to be taken back to school. Without bursaries, it is very worrying.

I congratulate the Members for seeing the essence of putting the little money that we had and slotting them in bursaries. I know and my fellow Hon. Members are witnesses that if there are many ECD classes done in every ward, they are two. Every Financial Year we have the ECD classes programme and I urge the Committee Members to do a thorough follow up for our core mandate in this Assembly is oversight.

When we get to know that there are things done the way they are not supposed to be done, we should know what else we can do. On the issue of pending bills, I do not know whether what is being told that Laikipia County is overworking we always slot money for pending bills but our brothers and sisters are out there. We do not know who are being paid. It is the high time we follow this budget to the letter.

If the budget is implemented well, we might not have delivered 100% but we shall be at 90% deliverance as we promised our people. With these few remarks I support the budget estimates and I urge H.E Governor to fast track and sign these bursaries then he starts the implementation of projects and we shall go far. Thank you, Madam Speaker.

Hon. Mutahi Muritu: Asante sana, Bi. Spika. Nasimama kutoa mchango wangu ikikumbukwa kwamba mwezi wa jana ulikuwa wa bajeti. Kile kitu ambacho kilikuwa kinanitia shaka ni tangu nichaguliwe kuwa mjumbe wa Bunge la Kaunti la Laikipia, kila mwaka Serikali Kuu kuna fedha ambazo tumekuwa tukipata kwa serikali.

Kwa mfano, mwaka wa 2017/2018 tulipata bilioni nne. Mwaka wa 2018/2019 tulipata bilioni moja, Mwaka wa 2019/2020 tulipata bilioni 1.177. Mwaka wa 2020/2021 tulipata bilioni nne kama mwaka wa 2017/2018 lakini mwaka wa 2021/2022 tunapata mgawo wa kawaida bila ruzuku zozote ambazo zinatoka kwa wawekezaji na washika dau wa maendeleo. Tumepata zaidi ya bilioni tano.

Bi Spika, ni heri kusema kile kilichoko rohoni mwa mtu. Ukiangalia bilioni tano na uchunguze sana, zaidi ya asilimia tisini na tano imeenda kulipa madeni. Swali ambalo najiuliza ni hizi bilioni zote nimesoma na bado naambiwa niko na deni huu ni mwaka wa mwisho nikiwa mjumbe.

Naomba wataalam wanisaidie watakapokuja na wakiweza kunisaidia waweze kunielewesha. Mwaka wa jana tulipitisha bilioni 4.1777. Ukifanya hesabu kwa sababu kila mtu

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

yuko na hii nyaraka, aende afanye hesabu yake na ajiulize hizo fedha zilienda wapi. Nimesonga na deni la zaidi bilioni nne mwaka mpya lakini hizo zingine zilizokusudiwa kufanyiwa kazi ziko wapi?

Bi. Spika, uchungu ninao kwa sababu leo asubuhi nilikutana na mtu mmoja ambaye ni mkandarasi. Aliniambia ya kwamba alijenga darasa kwangu ambayo tunaendelea kutumia na yeye alikuwa amekopa pesa. Alijenga barabara lakini bado hajalipwa. Tunapofuatilia taarifa kutoka kwa Serikali Kuu kutoka hazina, tunaelezwa ya kwamba hata lile kongamano la magavana katika nchi nzima walisema wiki jana kwamba tayari serikali kutoka hazina kuu imetoa bilioni mia tatu kumi na sita kwenye Kaunti.

Wajumbe tunajiuliza, hata kama sisi ni wajinga, hatuwi wajinga kwa sura zetu, angalau tuelezane kidogo na sio kwa ubaya. Hebu mtu ajisahili vizuri. Tumepewa bilioni tano lakini asilimia kubwa ya hizi pesa zitatumika kulipa madeni. Mwaka jana nilipewa pesa na serikali na mwaka huu mwingine pia na kila robo huwa tunaletewa ripoti. Kuna mkaguzi wa pesa za serikali na hilo ni swala la kujiuliza sana. Labda singejulikana isipokuwa ni wale wananchi kutoka Tigithi ambao walionileta hapa na pia hatungejuana na mtu yeyote. Mimi ningekuwa tu nachakaa nikikaa huko kijijini bila kujua chochote.

Waziri wa fedha mwenyewe alitoa taarifa ya kwamba tutakuwa makini zaidi kwa wale watu ambao hawatakuwa wamelipa watoa sabuni, kandarasi na huduma kwa bajeti ijayo. Sio mimi peke yangu na ukisikiliza kilichoko katika hili Bunge ni kwamba uchumi utakua kwa njia ipi? Uchumi unakua kunapokuwa mzunguko wa fedha. Tusipolipa yule mkandarasi, mzunguko wa pesa utatoka wapi hata kama sisi sio wataalamu wa kiuchumi? Sasa hivi tukienda hivi tukute wakandarasi kutoka Laikipia, bilioni tatu zimekaa na tunashindwa uchumi utakuwa namna gani.

Ndiyo tutaonekana saa zingine ni kama tunapinga lakini tujiulize swali ndogo tu. Mwaka jana tulijenga madarasa katika Kaunti yetu na tunapotoa ile kandarasi tunasema ya kwamba ni ya kina mama, walemavu na vijana. Hebu niambie, je yule mama mlemavu aliyeenda kwenye benki na kukopa milioni yake moja na akajenga darasa. Mimi nitajisifia sana kisiasa ya kwamba wadi yangu imejengwa, lakini yule mtu ambaye ni mlemavu hana hata senti.

Mimi najisifia sana ya kwamba nimejengea watu barabara lakini bado haijalipwa. Tuwache hayo mahali popote Gavana alipo. Nataka niwaambie ya kwamba hali ya hewa ya wanakandarasi wetu huko nje sio nzuri. Wale ambao wanapata makandarasi sio wa hii kaunti na kunaweza kuwa kwamba sio wawekezaji katika Kaunti yetu. Basi mzunguko wa fedha zetu za Laikipia na sisi ni walipa kodi, unapata katika wadi yetu tunafanya *projection* ya bilioni moja. Mwaka jana walisema ya kwamba waliokota karibu milioni mia tisa ambazo ni za walipa kodi wa Laikipia.

Maafisa tuliopatia vyeo na kuwapitisha katika hili Bunge letu, sasa tunaweza kuwa na usuhuba mwingine usiokuwa na tija kwa sababu mimi nitakuwa na usuhuba na yahe ya kwamba yeye ndiye alikuwa anasema. Lakini swali litakapoulizwa, halitaulizwa yule kwa sababu wewe ndiwe uliompa dhamana na sisi tumewapa vyeo, mawaziri na maafisa watendaji. Mwingine hapa alikuwa ananiambia ya kwamba wakati fulani ambapo watu hawakuwa wamepata dhamana ya kuwa katika hizo vyeo, walikuwa wanapokea simu. Sasa hivi hawapokei simu kwa sababu inakuwa wewe ni msumbufu kwa sababu shida imekulemea sana.

Nataka wapate hii taarifa kwa sababu cheo ni dhamana na hata mimi kuna wakati mwingine ninaweza kuwa nirudi ama nisirudi kwenye hili Bunge lakini nijiulize hata kwa mwenyezi Mungu, nilifanyia watu nini? Ni kweli ninapokea mafao yangu na kila kitu kingine lakini lazima nisimamie haki. Kile kitu ambacho kinaniuma sana, juzi nilipitia kwenye kituo

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

cha mafuta na nilikutana na ndugu fulani na akaniambia ya kwamba itabidi wafanye mgomo. Jana kulikuwa na tatizo na jana mwenyekiti wa bajeti aliuliza swali nyeti sana lakini linaanza kuonekana likiwa la kisiasa. Hujaweza kuonyesha hata nia ya madeni lakini unataka kukopa. Ni nani ambaye atakayekukopea?

Hatukatai deni, hata hii nchi yetu tunaishi kwa madeni kwa sababu makusudio yetu tunaweza kuwa tumesema ya kwamba tunataka kushakata maendeleo katika Kaunti yetu lakini kuwe na utaratibu. Kuna mama mmoja aliyejenga darasa akiwa na bwanake na ni mlemavu, hata napata aibu na sasa mimi nina uchungu. Kuna mwingine sasa hivi huwa ananililia akiniambia ya kwamba bwanake aliaga mwaka jana na alifanya kazi kwa kukopa pesa na bado hajalipwa. Sasa nashindwa, na sasa mimi ni Mheshimiwa wa aina gani ambaye hawezi kufuatilia haki ya mtu.

Leo asubuhi aliniambia ya kwamba kama yeye hatalipwa wiki ijayo, itabidi achotwe na unasikia ya kwamba yule mama ni yatima na mimi nilimwambia aje kwetu Laikipia ya kwamba tunajenga barabara. Ndiyo tunafanya maendeleo lakini wale wananchi wetu ili kupatikane mzunguko wa pesa, sasa hivi watu wakilipwa utaona mzunguko wa pesa kupitia maduka.

Tulipopitisha hiyo *leasing programme*, Bi. Spika, sitaki kukuambia lakini kuna wakati moja ulinilaumu na kuniambia ya kwamba mimi ndiye niliyekuwa mstari wa mbele kuipigia debe. Lakini sasa taarifa zinazotoka hapa sio zile ambazo tulikuwa tumeambiwa ya kwamba kutakuwa na vitengo vitano. Hata hizo vitengo tano hazionekani kwa miaka miwili, sasa kama vile Waheshimiwa kutoka Sosian na Mukogodo Mashariki walivyosema.

Ukiangalia vile Mheshimiwa kutoka Olmoran amesema, hii ifuatiliwe isiwe kwamba itatumika sehemu moja kwa sababu kama hiki kitu kinaongozwa na mtu mmoja na fedha zote zimewekwa pamoja, basi uwajibikaji uko wapi? Yule afisa ambaye alikuwa amesimamia hiyo *leasing programme* ni kijana mzuri sana na alipitia hapa tukaweza kumpa madaraka. Ukienda hata kwa ofisi yake atakuambia ya kwamba ako na nia njema ya kufanya kazi lakini anakwazika kwa sababu hana wa kumpokea kazi. Hata wale ambao wamepewa kandarasi bado hawapati mafao.

Ndugu zangu tuombeane dua na tumuombee hata kiongozi kwa sababu Mheshimiwa Gavana na hata sisi sio malaika lakini tujue ya kwamba cheo tulichopewa hapa, Mungu anatuona. Hawa watu wataendelea kufilisiwa na walijenga. Angalia madarasa, nimesikia Mheshimiwa George Meshami kutoka Mukogodo akielezea hali ya shule za chekechea katika Kaskazini mwa Laikipia na bado twapata ruzuku. Halafu ndugu zetu wananchi angalieni ruzuku na pesa za ziada ambazo tunapata na huitwa *Kenya Develution Support Programme* . Hizo fedha kalimani zinazohusika hatuziangalii kabisa na ni fedha nyingi sana ambazo zinatakikana kuweza kusongesha maendeleo na kukidhi bajeti.

Sasa nikitoka hapa kama Mheshimiwa Mutahi Muritu, itasemekana ya kwamba ni mimi ndiye nilikuwa nafanya. Hapana, mimi natetea kwa sababu ya ule uchungu ulioko kule mashinani. Kila mtu yuko na nyaraka yake, aende nayo na aisome na tuone tumepata pesa ngapi kwa hii miaka tano. Tuweze kuona, katika wadi yangu ni wangapi wanaodai. Serikali iliyopita, hakuna serikali ya kike na ya kiume, iliacha madeni na kuna watu ambao wanalia kwa sababu barabara zimeisha na tumezitumia sisi wote tunajivunia.

Bi. Spika, mimi naomba Wajumbe nisiwe mzungumzaji sana, sio eti ya kwamba sisi hatuna nia njema, tunayo. Kama sisi tumepata pesa kidogo sana katika Bunge letu ambazo ni milioni hamsini mwaka jana lakini sasa hivi ukienda utapata ofisi yenye heshima na hata kwa wadi zetu tumeweza kujenga maofisi. Hilo jambo Wabunge wa Laikipia ndicho mtakachojivunia katika huu muhula wa serikali ya pili kujenga makao makuu ya kila wadi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

katika Kaunti hii. Kwa hayo mengi au machache, naunga mkono ripoti hii na kila mtu na tuombe ili atusikilize vizuri na asikilize wananchi wetu. Siku zinazobaki, ndizo tunaendelea kubaki huku na kuenda kuomba ridhaa tena ili tuje tuwakilishe. Asante na ninaunga kutokana na kwamba niko hapa kwa niaba ya umma.

Hon. Simon Kanyutu: Thank you, Madam Speaker. I stand to support this report from the budget committee. The concern that Members are really raising is about pending bills. That is the challenge and I am sure that that is what we need to focus on. The issue pertaining to pending bills, even when we joined this Assembly there were some pending bills which had not been captured. In each and every department, we need to see how much should be allocated in each and every department to ensure that we leave a legacy whereby nobody will be left complaining.

I am happy because the Members have been able to peruse the document and are happy by the way it has been fixed and now the obligation is in absorption of this budget because this is our final year. A time like today I know that there will be nobody here but we will be outside there trying to see whether we will come back. The absorption of this budget matters a lot because there are some areas where Members have earmarked for development and now it depends on how absorption will be done. Because our role is oversight, we need to join hands and oversight to ensure that the work is done in the right way. I support.

Temporary Speaker (Hon. Catherine Nyawira): I now call upon the mover to reply

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bi. Spika. Kwanza nataka kushukuru Wajumbe wote kwa kutoa mchango wao kuhusu hii bajeti. Ukiangalia hali ilivyo katika hili Bunge, ni ya kwamba Wabunge wako na imani na kamati na bajeti ambayo inapitishwa siku ya leo. Kwa sababu ya kumbukumbu, ni vizuri kueleza ya kwamba pesa zote ambazo zinapitia kwa hii bajeti kwenda kwa wanalaikipia ni shilingi bilioni 8,137,999,410. Hizo ndizo pesa ambazo Kaunti ya Laikipia imeweza kupokea.

Bi. Spika, nafikiri ya kwamba Wabunge wameweza kutoa maoni yao na kueleza hisia zao na pia kushikana na kuongea kwa kauli moja ya kwamba haya mambo ya *bond* imekuwa ghali sana. Niseme kama Mheshimiwa Mutahi ya kwamba hata kama tumerarukiwa na nguo, bado hatujararukiwa na akili. Sioni vile unaweza kukopa bilioni moja halafu ulipe faida ya milioni 950 isipokuwa kuna mambo ingine imejificha huko ndani. Ndio maana hawa Wabunge wameona ni vizuri waweze kupitisha na kuiondoa kwa wakati huu ili tuweze kwanza kulipa yale madeni ambayo tuko nayo.

Juzi nilisema ya kwamba zile barabara nyingi ambazo zinatumiwa na wananchi wa Laikipia ni kukopwa zilikopwa kwa wananchi wa Laikipia wenyewe na hao wenyewe hawajalipwa yao. Tena twende tukope kwa wananchi wale wale wa Laikipia halafu tena tulipe faida kubwa kwa Wazungu. Kwa hivyo ukiangalia hiyo unaona ya kwamba hasaidii mwananchi wa Laikipia. Nafikiria hicho ndicho kitu ambacho serikali ya Laikipia ungefaa kufanya kwa sababu hauwezi kuwa na deni na unataka deni. Ni lazima kwanza ulipe deni ili upewe deni nyingine na hivyo ndivyo mambo huendelea.

Yule ambaye ametayarisha hii bajeti na kuileta ni Waziri wa Fedha. Ni vizuri tuelewe ya kwamba hii bajeti ilikuwa na shida kwa sababu haikuwa na pesa ya masomo ya ziada, barabara, maji na pia madawa. Hata kama haujui kuangalia vizuri, utaona ya kwamba huyu waziri anafanya mambo yake. Wakati mimi mwenyewe niliona hii bajeti nilijiuliza, huyu mtu ametengeneza bajeti kupitia kwa mawazo ya nani? Kwa sababu utawezaje kuleta bajeti hapa bila madawa ya hospitali? Labda wewe hauna roho ya wananchi. Mimi nimechaguliwa na

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wananchi na nimeletwa hapa na mwananchi. Yeye alikuja akatuuliza kazi na tukampatia na kwa hivyo anafaa kufanya vile sisi tunasema.

Kwa hivyo, hayo ndiyo maneno ambayo yako na hiyo ingine kutoka hapa kuendelea tutaweza kuulizana maswali kwa sababu ni vizuri wakati mwingine unapoanza kuuliza maswali hata wewe uwe tayari kwa yale hata wewe utaulizwa. Ni vizuri sasa nikomee hapo kwa mambo ya waziri ili tuendelee na hii ingine.

Mambo ya *leasing*, hapo ndipo shida ipo. Mwaka wa kwanza tulipopata huo mkataba, walikuwa wamewekea huu mpango wa *leasing* shilingi milioni 88,000,000 halafu wakapanda hadi milioni 90,000,000 na milioni 120,000,000 na sasa walikuwa wamepanda karibu milioni 160,000,000 ambayo iko juu sana ilhali yule mkataba wa kwanza tulikuwa tuwe na mitengo mitatu. *Excavator* tatu, tiba kumi na tano, *grader* tatu, *water bowser* tatu na *lowloader,* lakini hiyo pesa yote imetumika bila kuwa na hizo mashine zote.

Kwa hivyo tunapoendelea kuongeza pesa na hata mashine hazijaletwa, hata wakati mwingine huwa tunajiuliza mahali hii pesa huenda wapi au huwa inapelekwa kwa mfuko wa nani. Hii bajeti vile tumeipitisha, hakuna hata shilingi moja ambayo itapotea kwa sababu kila shilingi itaenda kwa kazi yake. Kila kazi lazima ifanyike na ndio maana hawa Wabunge wote kwa kauli moja wakaweza kupitisha hii pesa ili iweze kutumikia mwananchi wa kawaida ili aweze kupata maendeleo.

Jambo lingine kulingana na vile Wajumbe wamechangia, Mheshimiwa Catherine ameongea kuhusu Wadi ya Ngobit katika Bajeti kukosa barabara. Ninaona ya kwamba mambo ya barabara ipo katika hiyo ripoti katika idara ya Ujenzi na imepokea milioni 25,000,000 ambayo ni ya *road networks* na kwa hivyo, hiyo yote inaenda kwa wadi zote. Pengine ni jina tu ambalo haliko hapa na jina la Ngobit litawekwa na mtafuatilia ili mujue ya kwamba imewekwa ndani na iweze kufanyiwa kazi. Ikishawekwa ni vizuri muweze kufuatilia kama viongozi wa hiyo sehemu.

Bi. Spika, pesa nyingi tumepeleka kwa maendeleo ni pesa ambayo ilikuwa kwa *recurrent* ambayo haisaidii mwananchi kwa sababu mwananchi hasaidiki na *recurrent* lakini na maendeleo. Tumeonelea kama kamati tuondoe *recurrent* nyingi na tupeleke kwa maendeleo kwa sababu hizo *recurrent* ndizo huwa zinazunguka katika hii Laikipia zikitumika vibaya na zikitumika kwa kazi ambayo sio ya kusaidia mwananchi. Kwa hivyo hayo ndiyo mambo ambayo tuliweza kuonelea na kuweza kupitisha.

Leo tutapitisha hii bajeti ambayo iko na maji, madawa, barabara na pesa za ufadhili na ambayo pia itaweza kusaidia wananchi wa Laikipia. Jambo la kwanza Gavana wa Laikipia atakapofanya ni kuweza kuweka sahihi na kupelekea wananchi maendeleo. Wakati tunapopitisha bajeti kama Wabunge 24, Gavana yuko peke yake na kwa hivyo tuko na wananchi wengi zaidi na tunajua shida za wananchi zaidi. Kwa hivyo hatakuwa na jambo lingine ila tu kuweka sahihi hiyo stakabadhi na kupelekea wananchi maendeleo kwa sababu wakati mwingine huwa na kulaumiana wakisema ya kwamba ni Bunge ambayo haijapitisha.

Tunataka kusema kinagaubaga ya kwamba tumepitisha bajeti ili mwananchi afanyiwe kazi. Gavana anafaa aweke sahihi kama ako na roho ya mwananchi ndani yake ili watoto wasome, maji ipatikane na maendeleo ipatikane katika Laikipia. Kwa hayo machache Mungu awabariki, tuungane pamoja na tupitishe hii kwa kauli moja. Asante.

Temporary Speaker (Hon. Catherine Nyawira): I note that the ward representatives find this budget very inclusive and well distributed. The power of this House rests in the

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

committees which every one of us represents. So I want to urge the committees to ensure that this budget is oversighted well so that we can ensure that implementation is 100%.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Temporary Speaker (Hon. Catherine Nyawira): This House now stands adjourned until next week on Tuesday 20th July, 2021 at 2.30 p.m.

The House rose at 4.30 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*